



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na.MDC/CS.20/3VOLL.IV/21

Tarehe: 27 Julai,2023

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbogwe. Tangazo hili ni kutokana na kibali cha Ajira Mbadala chenye **Kumb Na. FA.170/521/01" B"119** cha tarehe **22.06.2023** kutoka kwa katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (**OR – UTUMISHI**)

### **MTENDAJI WA KIJIKI III – NAFASI NNE (04)**

#### **A. SIFA ZA MWOMBAJI**

- ❖ Awe amehitimu kidato cha nne (IV) au kidato cha sita (VI) mwenye mafunzo ya Astashahada/Cheti "NTA Level 5" katika moja wapo ya fani zifuatazo; -
- ❖ **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sanyasi ya Sanaa** kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **B. KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI**

- ❖ Kukusanya mapato ya halmashauri ya wilaya
- ❖ Afisa masuhuli na mtendaji mkuu wa serikali ya kijiji
- ❖ Kusimamia ulinzi na usalama wa rai ana mali zao, kuwa mlinzi wa amani, msimamizi wa utawala bora katika kijiji
- ❖ Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiji
- ❖ Katibu wa mikutano na kamati zote za Halmashauri ya Kijiji

- ❖ Kutafasiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- ❖ Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali
- ❖ Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya taaluma katika ngazi ya Kijiji
- ❖ Kusimamia kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Serikali ya Kijiji
- ❖ Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika Kijiji
- ❖ Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata
- ❖ Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri

### **C. NGAZI YA MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi ya mishahara ya Serikali **TGS B<sub>1</sub>**

### **D. MASHARTI YA JUMLA**

- a) Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri si zaidi ya miaka 45
- b) Barua ya maombi iambatane na wasifu binafsi wa mwombaji wa hivi karibuni (Curriculum Vitae)
- c) Barua ya maombi iambatanishwe na nakala ya vivuli vya vyeti vya Kidato cha nne (IV), Kidato cha sita (VI), Cheti cha kuzaliwa na Vyeti vingine vya Taaluma.
- d) Picha mbili ndogo (passport size) za hivi karibuni.
- e) Matokeo ya muda (Provisional/Testimonials/Statement of Results) Havikubaliki.
- f) Watumishi ambao ni waajiriwa wa serikali maombi yao lazima yalitishwe na waajiri wao wa sasa.
- g) Waombaji wenye vyeti vya kidato cha nne na sita waliosoma nje ya nchi wanatakiwa kuwasilisha uthibitisho wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA)
- h) Waombaji wenye vyeti vya Astashahada/Cheti vya nje ya nchi wanatakiwa kuambatanisha uthibitisho kutoka NACTE.
- i) Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- j) Mwombaji wa ajira atalazimika kuwa na namba ya utambulisho wa Uraia (National Identification Number) kutoka mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA).

- k) Mwisho wa kupokea Maombi ni Tarehe **13/08/2023 saa 9:30 Alasiri.**  
l) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili.

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA NJIA YA POSTA KWA;**  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBOGWE,  
S.L.P 01 MASUMBWE  
**MBOGWE.**

Imetolewa na:

  
Saada S. Mwaruka  
Mkurugenzi Mtendaji (W),  
MBOGWE

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**MBOGWE**